KCPE 2002

KISWAHILI

SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu kiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa una shaka, kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   NAMBA YAKO YA MTIHANI
   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika schemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

Katika kijitabu cha maswali:

21. Neno wimbo liko katika ngeli ya:

A. M-WA
B. U-N
C. M-MI
D. JI-MA

Jibu sahihi ni B.

Katika karatasi ya majibu:

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Maswali 1 mpaka 15.

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Mataifa yanayoendelea yahitajiwa __1__ wananchi kutilia maanani mipango ya kudhibiti uzazi na kupata watoto ambao wanapendeza __2__ ipasavyo. Ni jambo la busara kwa vijana __3__ vizuri kabla ya kufunga ndoa kuhusu jambo __4__ .

Hapo zamani za kale vijana __5__ kuhusu maisha ya ndoa na jamii. Vijana wa siku hizi nao wanahitaji kuongozwa. Hata hivyo, jambo la kusikitisha kuona kuwa __6__ wazazi wamewaachia walimu kazi hiyo. Hali kadhalika baadhi ya wazazi kuwa __7__ bora kwa wana, wengine wao ndio walio katika mstari wa mbele kuwapotosha __8__. Wazazi __9__ kujua kuwa vijana ndio tegemeo la taifa.

1.	A. yakiwazingatia	B. yakiwahimiza	C. yakihimizia	D. yakiwazingatia
2.	A. kuwatuza	B. kuwatuzia	C. kuwakidhi	D. kuwahamasisha
3.	A. kuwashauri	B. kushauriwa	C. kushurutishwa	D. kushurutika
4.	A. hiyo	B. hilo	C. hii	D. hizi
5.	A. walihusishwa	B. waliusiwa	C. walihusika	D. walitolewa
6.	A. miongoni mwa	B. baadhi ya	C. kati ya	D. baina ya
7.	A. kielezi	B. mwelekeo	C. kielelezo	D. maendelezo
8.	A. kwa vitendo vyao	B. na vitendo vyao	C. kwa vitendo yao	D. na vitendo yao
9.	A. hawana budi	B. hawanabudi	C. wana budi	D. wanabudi

__10__ hadi nyumbani kujipumzisha na kusubiri usiku ambao, kama usiku wa siku __11__ kulcta shangwe yoyote. Usiku __12__ ulifunika kila kitu na kurudisha hofu nyoyoni __13__ Kristina. Hali Hawakujua ni mambo __14__ ambayo yangewafika __15__ uchi hiyo ya majitu.

10.	A. Waliongoza	B. waliongozana	C. waliongozana	D. waliongozea
11.	A. ingine	B. ingineyo	C. linginelo	D. nyinginezo
12.	A. huu	B. hiyo	C. huo	D. hii
13.	A. kwa	B. ya	C. za	D. mwa
14.	A. ipi	B. yapi	C. yupi	D. zipi
15.	A. kwa	B. katika	C. juu ya	D. penye

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers Visit http://www.freekcpepastpapers.com
Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi:

16. Chagua uakifishi sahihi wa kifungu hiki yohana una nini mama alimwuliza
A. Yohana una nini? Mama alimwuliza
B. "Yohana una nini?" Mama alimwuliza
C. "Yohana una nini? Mama alimwuliza"
D. Yohana, una nini? Mama alimwuliza

17. Semi nyingine yenye maana sawa na:
Aliona kizunguzungu ni:
A. aliona kekeni
B. aliona rishi
C. aliona kisunzi
D. aliona kichefuchefu

18. Sentensi inayoonyesha wakati uliopita muda si mrefu ni:
A. Nilienda mapema na nikapongezwa
B. Huenda mapema na hupongezwa
C. Nimeenda mapema na nimepongezwa
D. Ninaenda mapema na ninapongezwa

19. Chagua sentensi inayoonyesha wingi wa:
Ufunguo wa nyumba ile umepotea
A. Funguo za nyumba hiyo zimepotea
B. Funguo za majumba yale zimepotea
C. Funguo za nyumba zile zimepotea
D. Funguo za nyumba hizo zimepotea

20. Chagua kiunganishi kifaacho kukamilisha sentensi hii:
Juma amefaulu mtihani wake _____ hajapata shule.
A. ndio
B. ila
C. pia
D. basi

21. Kanusha sentensi ifuatayo
Mkeka uliofumwa na mama uliuzwa
A. Mkeka usiofumwa na mama haujauzwa
B. Mkeka uliofumwa na mama hauuzwi
C. Mkeka ambao haukufumwa na mama haukuuzwa
D. Mkeka ambao haukufumwa na mama hautauzwa

22. Chagua sentensi ambayo si sahihi kuelezea:
Alinipigia simu
A. Alipiga simu pamoja na mwenzake kwa niaba yangu
B. Alinipasha ujumbe kupitia kwenye simu
C. Alikigonga chombo cha simu kwa niaba yangu
D. Alipitisha ujumbe kupitia kwa simu kwa niaba yangu

23. Chagua sentensi sahihi
A. Alifua samaki wengi
B. Alifua samaki nyingi
C. Alivua samaki wengi
D. Alivua samaki nyingi

24. Neno tamaa lina maana sawa na
A. hatia
B. shauku
C. uchoyo
D. wivu

25. Tambulisha jina la makundi lisilofaa
A. Kaumu ya watu
B. Kikosi cha watu
C. Halaiki ya watu
D. Umati wa watu

26. Chagua jibu lifaalo kuelezea maana ya methali:
Mchimba kisima huingia mwenyewe
A. Kisima ni hatari kwa aliyekichimba
B. Mtu akichimba kisima hutumbukia mwenyewe
C. Mtu akimwekea mtego mwenzake hujinasa mwenyewe
D. Mtu akichimba kisima huadhibiwa mwenyewe

27. Miereka ni:
A. mchezo wa kurukaruka
B. mchezo wa kupigana na kuangushana
C. mchezo wa mpira wa nyavu
D. mchezo wa kushikana na kuangushana

28. Kima ni nyama iliyosagwa, kima pia ni:
A. mnyama kama kobe
B. ndege wa angani
C. mnyama kama mjusi
D. aina ya nyani

29. Chagua sentensi inayoonyesha hali ya udogo ya sentensi:
Mbuzi wako aliyepotea amepatikana kwangu.
A. Kibuzi chako kilichopotea kimepatikana kwangu
B. Kibuzi wako aliyepotea amepatikana kwangu
C. Kibuzi chako aliyepotea amepatikana kwangu
D. Kibuzi yako iliyopotea imepatikana kwangu.

30. Kamilisha tashbihi
Kipofu kama _____
A. giza
B. fungo
C. kaburi
D. jongoo

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.

Kevin alikuwa mwenye bidii shuleni na hata nyumbani. Alimaliza kazi chapu chapu tena kwa usahihi. Ila yake kubwa ilikuwa husuda. Jane alikuwa mfanyi kazi kwa akina Kevin. 'Mbona wazazi wangu wanampa Jane pesa chungu nzima na mimi hata nilisaidia vipi sipewi japo senti moja? Kwa nini wazazi wakitoka, Jane anakuwa ndiye mkubwa wetu hapa? Wazazi wanamwamini sana, isitoshe wanamwachia pesa za matumizi. Lazima nitamchongea kwa wazazi afutwe kazi.' Kevin akaamua.

Siku moja, baada ya kufunga shule, Kevin alirudi nyumbani na matokeo mazuri ya mtihani. Alikuwa wa kwanza darasani. Wazazi wakafurahi na kumpongeza. Kevin aliona kuwa hiyo ilikuwa heko ya mdomo tu. Siku iliyofuata aliamua kuchoma nguru. Jane alijaribu juu chini kujitetea lakini aliambulia patupu. Kwa hakika ukweli wa mpitanjia si uongo wa mwenye nyumba. Akafunga virago vyake na kwenda zake akiwa amejawa na simanzi tele kwa kumwagiwa unga wake bure bilashi.

Asubuhi iliyofuata Kevin alidamka na kufanya kazi nyingi za ndani. Alipomaliza akatoka nje, akanaimifisha kiunga, akafua nguo na kupiga pasi. Akashughulikia maakuli ya mchana na kuandika meza. Aliwaita wadogo zake wakala na kuosha vyombo. Baadaye akawaambia wadogo zake waketi wasome. Wakamtii. Naye akafanya vivyo hivyo.

Punde si punde, Kevin akaanza kuhesabu kibunda chake cha siku. 'Leo nimefaulu kuwa mfanyi kazi bora kuliko Jane. Isitoshe, nimekuwa kiongozi hapa nyumbani na hata pesa za masurufu nilizopewa nimefaulu kuzitumia ipasavyo.' Baada ya hesabu ya uwongo na kweli, aling'amua kuwa siku hiyo angefaidika kwa kuzipata shilingi mia moja na hamsini. Hata hivyo mgongo wake ulimuuma ingawa ilikuwa tu siku ya kwanza. Aliamua kuwa kwa kazi zote alizofanya pamoja na usumbufu wa wadogo zake, angewahurumia wazazi kwa kuwadai shilingi mia moja tu. Malipo ya upishi hangewadai kwani ndio walionunua chakula. Mara akawaza, 'Niliwaletea wazazi ripoti nzuri sana mwisho wa muhula. Hivyo watanipa shilingi hamsini na zawadi juu yake.' Akajitia kusoma huku akitabasamu na kuwangojea wazazi kwa hamu na ghamu.

Wazazi walipowasili walistaajabu na kuuliza kama Jane alikuwa amerudi kwani nyumba ilikuwa ni safi sana. Kevin alifurahi akawapokea mizigo. Aliwajibu kuwa ndiye aliyefanya kazi hizo zote. Wazazi wakafurahi sana na kuwahimiza watoto wao wote kujifunza kazi za mikono kama Kevin.

Mara Kevin akaonyesha kusinywa kwani heko za mdomo tu zilikuwa kwake si kitu. Mkono mtupu haulambwi. Akawakabidhi wazazi ile orodha ya kazi alizozifanya akitarajia kibindo kizito ili awaringie nduguze. Wazazi walipoisoma, walitazamana kwa mshangao. Kisha wakamwita na kumketisha kitako wakampa pesa, akafurahi. Baadaye wakamwita na kumshauri, 'Sikiza vizuri. Sisi tulikuzaa, tukakulea kwa uchungu na gharama na bado tunaendelea kukutunza. Kwa hayo yote hatukudai na wala hatutakudai.'

Kevin kuyasikia hayo alifedheheka, akazijutia fikra zake finyu za kitoto. Alikuwa amesahau kwamba kuwasaidia wazazi ilikuwa ni jukumu lake. Alijuta kumwonea Jane wivu, akaomba msamaha kwa kumfitini. Aliwarudishia wazazi wake pesa walizokuwa wamempa.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

31. Jane alionewa wivu na Kevin kwa kuwa:
A. alifanya kazi vizuri akapendwa sana na wazazi
B. aliachiwa pesa za masurufu ingawa hakuwa mkubwa
C. alilipwa mshahara kwa kufanya kazi na kutunza watoto
D. Jane hakumpenda Kevin alipolipwa mshahara wake

32. Kevin alipofaulu hakutaka
A. kupongezwa tu bali apewe pesa na zawadi
B. heko ya wazazi pamoja na zawadi
C. apewe pongezi tu, zawadi na pesa
D. apewe pesa, zawadi, pamoja na pongezi

33. 'Ukweli wa mpita njia si uongo wa mwenye nyumba,' maana yake ni:
A. mwenye nyumba siku zote huaminika kwa kuwa ni mkweli
B. mwenyeji hata akiwa mbaya huaminiwa kuliko mgeni mkweli
C. mgeni hathaminiwi kwa kuwa ni mwongo kuliko mwenye nyumba
D. mgeni akisema ukweli huaminika kuliko mwenyeji asemaye ukweli

34. Kwa nini Kevin alitaka Jane aachishwe kazi?
A. ili Jane arudi kwao
B. ili Kevin asaidie wazazi
C. ili Kevin afaidike badala ya Jane
D. ili watoto wajifunze kazi

35. Wazazi walifurahi kwa sababu:
A. ingawa Jane alikuwa ameondoka kazi zote za nyumbani zilikuwa zimefanywa
B. nyumba ilikuwa safi ingawa Jane alikuwa ameondoka na siku hiyo wasingelipa chochote
C. watoto walikuwa wamesoma na Kevin aliyekuwa mkubwa aliomba pesa na kusema ukweli.
D. Kevin aliwapokea mizigo akawashukuru na akataka zawadi kwa kutunza watoto

36. <u>Akitarajia kibindo kizito</u> ina maana:
A. akitarajia apewe malipo makubwa kwa kazi zote alizofanya.
B. akitarajia apewe pesa kwa kazi alizofanya siku hiyo
C. akitarajia zawadi kwa kazi zote za siku alizofanya.
D. akitarajia kuhesabu pesa zote alizofanyia kazi siku hiyo

37. Kevin alivijutia vitendo vyake kwa kuwa
A. aliwadai wazazi wake malipo
B. ni wajibu wa wazazi kumfanyia makubwa
C. alikuwa mfanyi kazi bora kama Jane
D. aliumwa na mgongo siku ya kwanza

38. Neno lingine lenye maana sawa na neno <u>simanzi</u> ni:
A. hasira
B. kisasi
C. huzuni
D. wasiwasi

39. Ni mpango upi wa matendo ya Kevin ulio sawa kulingana na kifungu?
A. kuomba mshahara, kuchongea, kuomba msamaha, kufanya kazi.
B. kufanya kazi, kuchongea, kuomba mshahara, kuomba msamaha.
C. kuchongea, kufanya kazi, kuomba mshahara, kuomba msamaha.
D. kuomba msamaha, kufanya kazi, kuomba mshahara, kuchongea

40. Anwani ifaayo zaidi kwa habari hii ni:
A. Wajibu wa watoto na wazazi kwa wanao
B. Kevin kumwachisha Jane kazi
C. Jukumu la watoto kwa wazazi wao
D. Juhudi za Kevin nyumbani na shuleni

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.

Katika nchi nyingi zilizo maskini, vijana wengi wanaomaliza shule za msingi huridhika mapema. Wakikamilisha kiwango hicho hudhania kuwa wamepata elimu ya kutosha na wanaweza kufanya lolote. Wao husahau kuwa hicho walichosoma kilituvo kitone na kionjo tu cha bahari ya masomo.

Baadhi yao hufikiria kuwa wameikuwa watu wazima wafaao kuoa na kuolewa. Hawakumbuki kuwa 'watoto' wakianza kupata watoto tena bila kujiweza kifedha ni kujididimiza katika ufukara. Wengine husinywa na masomo wakidai kuwa wamechoka. Huu ni uvivu ulioje! Elimu ni bahari kubwa isiyokauka daima dawamu.

Jambo la kusikitisha ni kuwa, baadhi yao hupenda kuendelea na masomo lakini hawatii bidii. Wanadhani kuwa wazazi wao ni fukara mno. Kukata tamaa huku si kuzuri kamwe. Ni bora kusoma kwa bidii kwani tumeshawahi kuona watoto wengi maskini waliofaulu sana wakipata wadhamini. Ni heri kufa macho kuliko kukata tamaa. Mtu asomaye na kufaulu hata akikosa kwenda sekondari, bado atathaminiwa na jamii yake na ataitumia elimu hiyo kujiimarisha maishani.

Wengine hufaulu lakini shule huwa chache. Serikali inafanya juu chini kuongeza idadi ya shule. Vijana wanahimizwa wasome tu kwani hata kama watazikosa shule za upili wataweza kusomea kwenye vyuo vya ufundi. Kadhalika wanaweza kujiingiza katika masomo ya ngumbaru wakajisomea pole pole hadi chuo kikuu. Baada ya kumaliza wasipakate mikono na kusema kuwa hawatasoma tena. Wanapaswa kusoma magazeti, wasikilize taarifa za habari na ikiwezekana watazame runinga. Iwapo kuna maktaba za umma waende huko kusoma kwani ni rahisi sana mtu kuwa bongo-lala kama hasemi. Kinolewacho ndicho kipatacho.

Vijana wasiojiendeleza kielimu huweza kujiingiza kwa haraka katika anasa wasizozimudu. Maovu mengi huzidi nchini kama bongo hazitashughulishwa katika ujenzi wa taifa. Vijana watazidi kuwa kupe katika jamii badala ya kujitegemea. Mtegemea cha ndugu hufa maskini.

Nchi zote zinazotaka kutajika kuwa ni miongoni mwa mataifa yaliyoendelea lazima zihimize vijana wote wasome kwa bidii. Watobolewe ukweli kuwa kisomo hafifu hakimpeleki mtu popote. Umaskini uondolewe ili kila mtu aweze kusomesha wanawe. Ikibidi kisomo kiwe cha lazima hadi kidato cha pili au cha nne. Hili likikubalika, wanafunzi hawatakua tu kinwili bali kiakili pia. Matendo yao yatakuwa yanaonyesha busara zaidi na watajiendeleza kiuchumi. Ukosefu wa elimu ni hatari kwa usalama kwani huchangia kuongeza ujinga, umaskini na magonjwa.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

41. Hatari ya 'watoto' kupata watoto ni:
A. kuzama katika uhalifu
B. kuchoshwa na masomo
C. kujiingiza katika umaskini
D. kufukuzwa na wazazi

42. Wanafunzi wengine chaweni bidii kwa sababu
A. hukata tamaa na kutoroka
B. hata wakipita hawatapata shule na vyuo
C. wanadhani wakipita wazazi hawatapata karo
D. wanadhani wazazi wao watawaoza mara moja

43. Maana ya elimu ni bahari kubwa isiyokauka mima dawamu ni
A. elimu ya shuleni ina kina kirefu
B. elimu ya shuleni ni bahari kubwa
C. elimu haina kikomo
D. elimu huleta maarifa

44. Tatizo linalowakabili wanafunzi wengine waliofaulu ni:
A. uhaba wa vyuo vya ufundi
B. ukosefu wa shule za kutosha
C. kukosa runinga na magazeti
D. kusomea shule za ufundi

45. Kukosa kujiendeleza kielimu huwafanya vijana
A. kusugua bongo
B. kuwa wategemezi
C. kuwa watu wakubwa
D. kusoma katika maktaba

46. Mataifa yanayoendelea
A. lazima yawe macho shuleni
B. lazima yahimize kisomo kwa wote
C. lazima yawe na matendo ya busara
D. lazima yatajike miongoni mwa mataifa mengine

47. Wadhamini ni
A. wanaohimiza
B. wanaoheshimu
C. wanaosaidia
D. wanaotuliza

48. Vijana wanapaswa kusoma magazeti na kusikiliza habari ili
A. waburudike vilivyo
B. wapanue mawazo
C. wasiingie katika anasa
D. wasiwe walegevu

49. Ni jibu gani lisilo sawa kulingana na kifungu ulichosoma?
A. vijana wasiojiunga na shule za sekondari wanaweza kusoma elimu ya ngumbaru
B. vijana wote waliokosa nafasi ya kujiendeleza kimasomo hapa nchini wamejiingiza katika maovu.
C. vijana wengi wakimaliza masomo ya msingi huridhika.
D. vijana wengine hawatii bidii shuleni

50. Maana ya msemo, Kinolewacho ndicho kipatacho ni
A. kinachotiwa makali hukata
B. kinachoimarishwa kila mara hufaa
C. kinachotengenezwa hupata makali
D. Kinachonolewa hupewa heko.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.